

HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI

Simuyamdomo 027 2977402
Tel Fax: 027 2977402
Email: ded@handenidc.go.tz
Tovuti: www.handenidc.go.tz



Ofisiya Mkurugenzi
Mtendaji (W)
S.L.P. 355,
Handeni
Tanga,

TAARIFA KWA UMMA .

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Bw. William Makufwe amewatakiwa mitihani mema wanafunzi wote wanaofanya mtihani wa taifa kuanzia leo Octoba 30 na kuwataka kuwa watulivu kwa kufuata maelekezo wanayopewa na wasimamizi wao kipindi chote cha mitihani yao.

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kwa mwaka 2017 ina jumla ya watahiniwa 1024 ambapo watahiniwa wa shule wavulana 476 na wasichana 515, watahiniwa binafsi(PC) wavulana 12 na wasichana 19, watahiniwa wa maarifa (QT) msichana 1 na mvulana 1 na kufanya jumla ya watahiniwa wote 1024 kwa wavulana 489 na wasichana 535.

Watahiniwa wa shule vituo vya kufanyia mtihani ni 21, watahiniwa binafsi na watahiniwa wa maarifa kituo ni kimoja cha Kabuku, ambapo pia kati ya shule 24 za sekondari za Halmashauri ya Wilaya ya Handeni shule 3 hazitafanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne kwa sababu ya kutofikia hatua ya kuwa na wanafunzi wa kidato cha nne.

Idadi ya watahiniwa kwa mwaka 2017 imeshuka sababu ya utoro na kuhama mazingira ya Handeni tofauti na mwaka 2016 ambapo jumla ya watahiniwa 1277 wavulana 633 na wasichana 644 walisajiliwa kufanya mitihani wa kuhitimu kidato cha nne.

IMEANDALIWA :

KITENGO CHA TEKNOLOJIA, HABARI NA MAWASILIANO
HALMASHAURI YA WILAYA HANDENI

30/10/2017